OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR

# TOLEO LA TAKWIMU ZA AJALI NA MAKOSA YA BARABARANI ZANZIBAR, MWAKA 2025

## OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

## Utangulizi

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ajali na makosa ya barabarani. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11).


## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

## Ajali za Barabarani

Jumla ya ajali 260 zimeripotiwa mwaka 2025. Wilaya ya Kaskazini “B” imeripotiwa kuwa na ajali nyingi (ajali 43) sawa na asilimia 16.5 ikilinganishwa na wilaya nyengine.


**Kielelezo 1.1: Idadi ya Ajali za Barabarani Kwa Wilaya, Mwaka 2025**




Idadi ya Ajali za barabarani zilizotokea mwaka 2025 zimeongezeka kwa asilimia 17.1 kufikia ajali 260 kutoka ajali 222 mwaka 2024


Mwaka 2025, wilaya ya Kaskazini “B” imeripotiwa kuwa na ajali zaidi (ajali 43) ikilinganishwa na ajali 38 zilizoripotiwa kutoka wilaya ya Kaskazini “A” kwa mwaka 2024.

**Kielelezo 1.2: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani kwa Mwaka 2024 na Mwaka 2025**




Jumla ya waathirika 441 wameripotiwa mwaka 2025, ambapo waathirika 397 ni wanaume na waathirika 44 ni wanawake. Wilaya ya Kaskazini "B" imeripotiwa kuwa na waathirika wengi (waathirika 78) sawa na asilimia 17.7 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Mwaka 2025**





Waathirika waliofariki mwaka 2025 wameongezeka kwa asilimia 17.5 kufikia waathirika 222 kutoka waathirika 189 mwaka 2024. Wilaya ya Magahribi 'A' imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya waathirika waliofariki mwaka 2025 (waathirika 38) vilevile mwaka 2024 (waathirika 36).

**Kielelezo 1.4: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwaka 2024 na Mwaka 2025**





Waathirika waliojeruhiwa mwaka 2025 wamepungua kwa asilimia 2.2 na kufikia waathirika 219 kutoka waathirika 224 mwaka 2024. Wilaya ya Kaskazini 'A' na Kaskazini 'B' zimeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya waathirika waliojeruhiwa mwaka 2025 (waathirika 52 kila wilaya) ikilinganishwa na waathirika 42 walioripotiwa kutoka wilaya ya Kaskazini 'A' mwaka 2024

**Kielelezo 1.5: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwaka 2024 na Mwaka 2025**




Mwaka 2025 miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani (waliojeruhiwa na waliofariki), waathirika wengi wameonekana ni abiria (waathirika 186), wapanda baiskeli na pikipiki 163, waenda kwa miguu 69 na madereva walikuwa 23

**Kielelezo 1.6: Idadi na Aina ya Waathirika wa Ajali za barabarani, Mwaka 2025**





Mwaka 2025, ajali nyingi zilitokea muda wa saa 12:01 jioni hadi saa 03:00 usiku ambapo zimeripotiwa ajali 54

**Kielelezo 1.7: Idadi ya Ajali na Muda Uliotokea, Mwaka 2025**




Kati ya ajali 260 zilizoripotiwa mwaka 2025, ajali 194 zimesababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi na ajali 66 zimesababishwa na uzembe wa dereva. Mkoa wa Mjini Magharibi umekuwa na ajali nyingi zilizosababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi (ajali 64) na Mkoa wa Kaskazini Unguja umekuwa na ajali nyingi zilizosababishwa na Uzembe wa madereva (ajali 28).

**Kielelezo 1.8: Chanzo cha Ajali za Barabarani kwa Mkoa, Mwaka 2025**.




## Makosa ya Barabarani

Jumla ya makosa 70,751 yameripotiwa mwaka 2025, ambapo makosa 70,665 yameripotiwa kwa wanaume na makosa 86 yameripotiwa kwa wanawake.

Wilaya ya Mjini imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa 12,984) sawa na asilimia 18.4 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa. Wilaya ya Micheweni ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani yaliyoripotiwa ambayo ni makosa 572 (asilimia 0.8) kati ya makosa yote yaliyoripotiwa.


**Kielelezo 2.0: Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Wilaya, Mwaka 2025**




Kosa kuu lililoripotiwa mwaka 2025 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 30,798) yakifuatia Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo (makosa 17,224) na Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia (makosa 8,354).

Orodha ya makosa haya matatu (3) ya barabarani kati ya yote kumi na moja (11) yaliyoripotiwa mwaka 2025 yamechangia asilimia 79.7


**Kielelezo 2.1: Idadi na Aina ya Makosa ya Barabarani, Mwaka 2025**



Idadi ya makosa kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 49.7 na kufikia makosa 70,751 mwaka 2025 kutoka makosa 47,258 mwaka 2024.

Wilaya ya Mjini ilikuwa na idadi kubwa ya makosa mwaka 2025 (Makosa 12,984) na wilaya ya Magharibi ‘A’ ilikuwa na idadi kubwa ya makosa mwaka 2024 (makosa 7,836).

**Kielelezo 2.2: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani kwa mwaka 2024 na mwaka 2025**



## HITIMISHO

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11). Lengo la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar.

Jumla ya ajali 260 zimeripotiwa mwaka 2025. Wilaya ya Kaskazini "B" imeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni 43 sawa na asilimia 16.5 ikilinganishwa na wilaya nyengine

Mlinganisho wa idadi ya ajali za barabarani zilizotokea mwaka 2025 zimeongezeka kwa asilimia 17.1 kufikia ajali 260 mwaka 2025 kutoka ajali 222 mwaka 2024

Jumla ya makosa 70,751 yameripotiwa mwaka 2025, ambapo makosa 70,665 yameripotiwa kwa wanaume na makosa 86 yameripotiwa kwa wanawake.

Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwaka 2025 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa **30,798**) sawa na asilimia 43.5 ya makosa yote yaliyoripotiwa mwaka 2025.

## Kiambatanisho:

**Jadweli 3.0: Idadi na Asilimia ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Mwaka 2025**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waliokufa | | | | Waliojeruhiwa | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nambari | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia |
| Kaskazini 'A' | 29 | 11.2 | 18 | 2 | 20 | 9.0 | 36 | 16 | 52 | 23.7 | 54 | 18 | 72 | 16.3 |
| Kaskazini 'B' | 43 | 16.5 | 25 | 1 | 26 | 11.7 | 50 | 2 | 52 | 23.7 | 75 | 3 | 78 | 17.7 |
| Kati | 37 | 14.2 | 30 | 3 | 33 | 14.9 | 22 | 1 | 23 | 10.5 | 52 | 4 | 56 | 12.7 |
| Kusini | 20 | 7.7 | 17 | 0 | 17 | 7.7 | 13 | 0 | 13 | 5.9 | 30 | 0 | 30 | 6.8 |
| Mjini | 17 | 6.5 | 12 | 5 | 17 | 7.7 | 3 | 0 | 3 | 1.4 | 15 | 5 | 20 | 4.5 |
| Magharibi 'A' | 35 | 13.5 | 37 | 1 | 38 | 17.1 | 10 | 1 | 11 | 5.0 | 47 | 2 | 49 | 11.1 |
| Magharibi 'B' | 28 | 10.8 | 26 | 0 | 26 | 11.7 | 15 | 1 | 16 | 7.3 | 41 | 1 | 42 | 9.5 |
| Wete | 15 | 5.8 | 10 | 2 | 12 | 5.4 | 18 | 1 | 19 | 8.7 | 28 | 3 | 31 | 7.0 |
| Micheweni | 10 | 3.8 | 6 | 3 | 9 | 4.1 | 16 | 0 | 16 | 7.3 | 22 | 3 | 25 | 5.7 |
| Chake chake | 17 | 6.5 | 13 | 2 | 15 | 6.8 | 6 | 2 | 8 | 3.7 | 19 | 4 | 23 | 5.2 |
| Mkoani | 9 | 3.5 | 8 | 1 | 9 | 4.1 | 6 | 0 | 6 | 2.7 | 14 | 1 | 15 | 3.4 |
| **Zanzibar** | **260** | **100** | **202** | **20** | **222** | **100** | **195** | **24** | **219** | **100** | **397** | **44** | **441** | **100** |

### Jadweli 3.1: Idadi ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Mwaka 2025

| Wilaya | Idadi ya Ajali | Dereva | | | | | | Abiria | | | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | | | Waendao kwa Miguu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wa liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Wa liokufa | | | Waliojeruhiwa | | |
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Kaskazini 'A' | 29 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 9 | 2 | 11 | 24 | 14 | 38 | 4 | 0 | 4 | 10 | 1 | 11 | 3 | 1 | 4 | 2 | 1 | 3 |
| Kaskazini 'B' | 43 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 3 | 9 | 0 | 9 | 30 | 2 | 32 | 12 | 1 | 13 | 8 | 0 | 8 | 3 | 0 | 3 | 9 | 0 | 9 |
| Kati | 37 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 7 | 0 | 7 | 10 | 1 | 11 | 16 | 1 | 17 | 7 | 0 | 7 | 5 | 2 | 7 | 4 | 0 | 4 |
| Kusini | 20 | 4 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 7 | 0 | 7 | 7 | 0 | 7 | 6 | 0 | 6 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 17 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 | 5 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 3 | 0 | 3 | 4 | 1 | 5 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 35 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 8 | 1 | 9 | 1 | 1 | 2 | 18 | 0 | 18 | 5 | 0 | 5 | 10 | 0 | 10 | 2 | 0 | 2 |
| Magharibi 'B' | 28 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 6 | 12 | 1 | 13 | 14 | 0 | 14 | 2 | 0 | 2 | 5 | 0 | 5 | 1 | 0 | 1 |
| Wete | 15 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 4 | 10 | 1 | 11 | 4 | 0 | 4 | 6 | 0 | 6 | 2 | 0 | 2 | 2 | 0 | 2 |
| Micheweni | 10 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 7 | 0 | 7 | 3 | 1 | 4 | 6 | 0 | 6 | 1 | 2 | 3 | 1 | 0 | 1 |
| Chake chake | 17 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 3 | 2 | 5 | 12 | 0 | 12 | 4 | 0 | 4 | 3 | 1 | 4 | 4 | 0 | 4 |
| Mkoani | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 4 | 2 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **260** | **15** | **0** | **15** | **8** | **0** | 8 | **48** | **10** | **58** | **105** | **22** | **127** | **99** | **5** | **104** | **57** | **1** | **58** | **38** | **7** | **45** | **25** | **1** | **26** |

**Jadweli 3.2: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwaka 2024 na Mwaka 2025**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 |
| Kaskazini 'A' | 38 | 29 | 42 | 52 | 28 | 20 | 0 | 0 | 1 | 1 | 23 | 38 | 4 | 11 | 11 | 11 | 13 | 4 | 8 | 3 | 10 | 4 |
| Kaskazini 'B' | 29 | 43 | 38 | 52 | 19 | 26 | 3 | 3 | 0 | 1 | 30 | 32 | 4 | 9 | 4 | 8 | 11 | 13 | 1 | 9 | 4 | 3 |
| Kati | 24 | 37 | 18 | 23 | 19 | 33 | 2 | 1 | 2 | 2 | 5 | 11 | 6 | 7 | 11 | 7 | 4 | 17 | 0 | 4 | 7 | 7 |
| Kusini | 12 | 20 | 26 | 13 | 12 | 17 | 1 | 0 | 2 | 4 | 20 | 7 | 2 | 4 | 1 | 6 | 6 | 7 | 4 | 0 | 2 | 2 |
| Mjini | 10 | 17 | 3 | 3 | 10 | 17 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 5 | 0 | 3 | 7 | 5 | 1 | 0 | 3 | 5 |
| Magharibi 'A' | 33 | 35 | 31 | 11 | 36 | 38 | 2 | 2 | 2 | 1 | 19 | 2 | 14 | 9 | 5 | 5 | 9 | 18 | 5 | 2 | 11 | 10 |
| Magharibi 'B' | 32 | 28 | 16 | 16 | 23 | 26 | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 | 13 | 2 | 6 | 7 | 2 | 9 | 14 | 5 | 1 | 12 | 5 |
| Wete | 12 | 15 | 12 | 19 | 12 | 12 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 11 | 1 | 4 | 9 | 6 | 7 | 4 | 1 | 2 | 4 | 2 |
| Micheweni | 13 | 10 | 21 | 16 | 11 | 9 | 0 | 2 | 0 | 1 | 13 | 7 | 2 | 1 | 5 | 6 | 3 | 4 | 3 | 1 | 6 | 3 |
| Chake chake | 12 | 17 | 12 | 8 | 14 | 15 | 1 | 0 | 0 | 0 | 7 | 5 | 3 | 2 | 3 | 4 | 10 | 12 | 1 | 4 | 1 | 4 |
| Mkoani | 7 | 9 | 5 | 6 | 5 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 6 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| **Zanzibar** | **222** | **260** | **224** | **219** | **189** | **222** | **9** | **8** | **7** | **15** | **127** | **127** | **38** | **58** | **59** | **58** | **82** | **104** | **29** | **26** | **62** | **45** |

## Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa Kwa Wilaya na Jinsi, Mwaka 2025

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | | Uendeshaji Hatari | | | Ubovu wa Vipando | | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 32 | 0 | 32 | 10 | 0 | 10 | 48 | 0 | 48 | 375 | 0 | 375 | 2,430 | 0 | 2,430 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 36 | 0 | 36 | 420 | 0 | 420 | 2,573 | 0 | 2,573 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 593 | 0 | 593 | 531 | 0 | 531 | 414 | 0 | 414 | 2,003 | 2 | 2,005 | 2,316 | 0 | 2,316 |
| Kusini | 30 | 0 | 30 | 42 | 0 | 42 | 333 | 0 | 333 | 379 | 0 | 379 | 860 | 0 | 860 | 3,024 | 0 | 3,024 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 7 | 413 | 0 | 413 | 1,260 | 0 | 1,260 | 1,922 | 0 | 1,922 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 640 | 0 | 640 | 1,436 | 0 | 1,436 | 2,452 | 0 | 2,452 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 346 | 0 | 346 | 1,065 | 0 | 1,065 | 1,552 | 0 | 1,552 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 50 | 0 | 50 | 13 | 0 | 13 | 61 | 0 | 61 | 337 | 0 | 337 | 222 | 0 | 222 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 | 9 | 67 | 0 | 67 | 139 | 0 | 139 | 225 | 0 | 225 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 16 | 0 | 16 | 71 | 0 | 71 | 284 | 25 | 309 | 294 | 2 | 296 | 273 | 0 | 273 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 19 | 5 | 24 | 20 | 0 | 20 | 187 | 48 | 235 | 157 | 4 | 161 | 235 | 0 | 235 |
| **Zanzibar** | **30** | **0** | **30** | **752** | **5** | **757** | **1,006** | **0** | **1,006** | **2,875** | **73** | **2,948** | **8,346** | **8** | **8,354** | **17,224** | **0** | **17,224** |

**Inaendelea… Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa kwa Wilaya na Jinsi, Mwaka 2025**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani yammiliki wa gari | | | Kughushi nyaraka za serikalikwa gari za abiria | | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gariza abiria | | | Kutofuata miongozo na kanuniza usalama barabarani | | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawilikwenye Chombo za Maringi Mawili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 375 | 0 | 375 | 4286 | 0 | 4286 | 44 | 0 | 44 | 7,600 | 0 | 7,600 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 793 | 0 | 793 | 4900 | 0 | 4900 | 20 | 0 | 20 | 8,744 | 0 | 8,744 |
| Kati | 495 | 0 | 495 | 409 | 0 | 409 | 953 | 0 | 953 | 662 | 0 | 662 | 414 | 0 | 414 | 8,790 | 2 | 8,792 |
| Kusini | 165 | 0 | 165 | 0 | 0 | 0 | 1,012 | 0 | 1,012 | 329 | 0 | 329 | 74 | 0 | 74 | 6,248 | 0 | 6,248 |
| Mjini | 1,065 | 0 | 1,065 | 0 | 0 | 0 | 714 | 0 | 714 | 7,603 | 0 | 7,603 | 0 | 0 | 0 | 12,984 | 0 | 12,984 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 782 | 0 | 782 | 6,402 | 0 | 6402 | 0 | 0 | 0 | 11,712 | 0 | 11,712 |
| Magharibi 'B' | 557 | 0 | 557 | 244 | 0 | 244 | 537 | 0 | 537 | 5,837 | 0 | 5,837 | 0 | 0 | 0 | 10,148 | 0 | 10,148 |
| Wete | 53 | 0 | 53 | 0 | 0 | 0 | 275 | 0 | 275 | 304 | 0 | 304 | 26 | 0 | 26 | 1341 | 0 | 1,341 |
| Micheweni | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 36 | 0 | 36 | 83 | 0 | 83 | 11 | 0 | 11 | 572 | 0 | 572 |
| Chake chake | 35 | 0 | 35 | 11 | 0 | 11 | 279 | 0 | 279 | 221 | 0 | 221 | 12 | 0 | 12 | 1,496 | 27 | 1,523 |
| Mkoani | 14 | 0 | 14 | 39 | 0 | 39 | 169 | 0 | 169 | 162 | 0 | 162 | 28 | 0 | 28 | 1,030 | 57 | 1,087 |
| **Zanzibar** | **2,386** | **0** | **2,386** | **703** | **0** | **703** | **5925** | **0** | **5925** | **30,789** | **0** | **30,789** | **629** | **0** | **629** | **70,665** | **86** | **70,751** |

**Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Mwaka 2024 na Mwaka 2025**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha motobila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni,bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 8 | 32 | 82 | 10 | 47 | 48 | 974 | 375 | 1,236 | 2,430 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 23 | 0 | 30 | 2 | 103 | 36 | 1,393 | 420 | 1,987 | 2,573 |
| Kati | 0 | 0 | 153 | 593 | 578 | 531 | 565 | 414 | 1,013 | 2,005 | 1,331 | 2,316 |
| Kusini | 0 | 30 | 107 | 42 | 289 | 333 | 608 | 379 | 697 | 860 | 801 | 3,024 |
| Mjini | 0 | 0 | 119 | 0 | 0 | 7 | 219 | 413 | 893 | 1,260 | 1,268 | 1,922 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 65 | 0 | 194 | 0 | 473 | 640 | 859 | 1,436 | 1,314 | 2,452 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 55 | 0 | 74 | 10 | 242 | 346 | 685 | 1,065 | 1,059 | 1,552 |
| Wete | 0 | 0 | 31 | 50 | 20 | 13 | 85 | 61 | 525 | 337 | 173 | 222 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 9 | 53 | 67 | 221 | 139 | 268 | 225 |
| Chake chake | 1 | 0 | 9 | 16 | 23 | 71 | 372 | 309 | 410 | 296 | 348 | 273 |
| Mkoani | 0 | 0 | 23 | 24 | 23 | 20 | 256 | 235 | 231 | 161 | 285 | 235 |
| **Zanzibar** | **1** | **30** | **593** | **757** | **1330** | **1006** | **3,023** | **2948** | **7,901** | **8,354** | **10,070** | **17,224** |


**Inaendelea… Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Mwaka 2024 na Mwaka 2025**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Kutofunga Namba mbele ya Chombo cha Moto | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 | Mwaka 2024 | Mwaka 2025 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 491 | 375 | 1,770 | 4,286 | 15 | 44 | 0 | 0 | 4623 | 7,600 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 644 | 793 | 2,930 | 4,900 | 17 | 20 | 0 | 0 | 7127 | 8,744 |
| Kati | 178 | 495 | 81 | 409 | 1,848 | 953 | 660 | 662 | 339 | 414 | 0 | 0 | 6746 | 8,792 |
| Kusini | 91 | 165 | 0 | 0 | 739 | 1,012 | 496 | 329 | 238 | 74 | 0 | 0 | 4066 | 6,248 |
| Mjini | 186 | 1,065 | 25 | 0 | 554 | 714 | 3,201 | 7,603 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6465 | 12,984 |
| Magharibi 'A' | 134 | 0 | 81 | 0 | 564 | 782 | 4,152 | 6,402 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7836 | 11,712 |
| Magharibi 'B' | 172 | 557 | 27 | 244 | 553 | 537 | 2,437 | 5,837 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5304 | 10148 |
| Wete | 13 | 53 | 8 | 0 | 115 | 275 | 309 | 304 | 7 | 26 | 0 | 0 | 1286 | 1,341 |
| Micheweni | 18 | 2 | 0 | 0 | 79 | 36 | 62 | 83 | 0 | 11 | 0 | 0 | 718 | 572 |
| Chake chake | 18 | 35 | 77 | 11 | 228 | 279 | 297 | 221 | 25 | 12 | 0 | 0 | 1808 | 1,523 |
| Mkoani | 3 | 14 | 10 | 39 | 230 | 169 | 173 | 162 | 45 | 28 | 0 | 0 | 1279 | 1,087 |
| **Zanzibar** | **813** | **2,386** | **309** | **703** | **6,045** | **5,925** | **16,487** | **30,789** | **686** | **629** | **0** | **0** | **47,258** | **70,751** |


**Jadweli 3.7 Tozo zilizolipwa Mahakamani Kwa Wilaya na Idadi ya kesi, Mwaka 2025**

| Wilaya | Idadi ya kesi | Tozo(Shilingi) |
|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 7,635 | 200,291,747 |
| Kaskazini 'B' | 8,668 | 225,873,723 |
| Kati | 8,318 | 327,663,850 |
| Kusini | 6,240 | 208,130,450 |
| Mjini | 13,042 | 371,099,000 |
| Magharibi 'A' | 12,706 | 368,236,400 |
| Magharibi 'B' | 9,932 | 289,883,225 |
| Wete | 1,349 | 22,861,000 |
| Micheweni | 609 | 9,859,600 |
| Chake chake | 1,521 | 27,374,610 |
| Mkoani | 1,135 | 21,378,990 |
| **Zanzibar** | **71,155** | **2,072,652,595** |

**Kielelezo1: Ajali za Barabarani Zilizoripotiwa kwa Wilaya, Mwaka, 2025**



**Kielelezo 2: Vifo na Majeruhi Wanaotokana na Ajali za Barabarani kwa Wilaya Mwaka, 2025**



## Zingatia Maelezo

Ajali ya barabarani inahusu ajali yeyote inayohusisha angalau gari moja barabarani, inayotokea barabarani kwa mzunguko wa umma na angalau mtu mmoja amekufa au amejeruhiwa. Kutokana na Sheria ya Adhabu nambari.6/2004 kuondoa Amri ya Adhabu, sura ya 13 ya sheria ya Zanzibar (Penal Act no. 6/2004 Act to repeal the Penal Decree, chapter 13 of the law of Zanzibar).

Kifo imefafanua iwapo kama watu wamepata ajali na kufa papo hapo au ndani ya mwaka mmoja na siku moja (366) baada ya ajali.

Watu waliojeruhiwa na waathirika kwa ajali waliopatwa na mshtuko wanaohitaji matibabu ya Hospitali au bila hospitali.

Njia kimsingi ina maana ya usafiri. Hio humpa binadamu kufikia maeneo tofauti. Watu wengi hutumia njia tofauti za usafiri. Baadhi yao hutumia gari, baiskeli na kwa miguu.

Kosa ni uhalifu ambao huvunja sheria fulani na kuwepo adhabu maalum. Ajali za barabarani husababishwa na makosa mbalimbali ya binadamu. Makosa mengi ambayo yanaonekana kuwa ni madogo lakini athari yake inakuwa kubwa. Matokeo yake watu hupata ulemavu au kufa.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua, 2321,
Simu: +255242231869,
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com,
Nukushi: 024223136,
MMP, Zanzibar